

Live for today,
Learn from yesterday,
Hope for tomorrow.

Wanafunzi walishiriki katika Akademia ya mapumziko ya majira ya masika wakati wa likizo ya Aprili kusaidia kujitayarisha kwa majaribio.

MIUNGANISHO

APRILI 14, 2023

KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI

DKT. JAVIER MONTAÑEZ
MSIMAMIZI MKUU

Karibu kwenye toleo jipya la Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence (PPSD) kijarida cha mara mbili kwa wiki! Ikiwa wewe au mtu unayemjua atakosa mojawapo ya vijarida vyetu, unaweza kupata matoleo ya awali kwenye tovuti ya Wilaya katika lugha nyingi.

SurveyWorks, SurveyWorks, SurveyWorks! Asanteni nyote kwa wale waliochukua muda wao kukamilisha utafiti huu. Tunategemea maono yenu yatuongoze wakati tunapofanya kazi pamoja kubadilisha Wilaya. Tuli pitisha lengo letu kwa kiwango cha 39% cha kukamilisha kupitia familia zetu. Hatungeweza kufanya kile tunacho fanya bila wewe.

Weka alama katika kalenda zenu! PSAT na SAT zitafanyika Aprili tarehe 19. Majaribio ya RICAS Sanaa ya Lugha ya Kiingereza (ELA) ni April tarehe 18 hadi tarehe 20 kwa wanafunzi wetu wa darasa la 3 - 8. Majaribio ya RICAS ya hisabati yatakuwa May tarehe 15 hadi 19.

Ilikuwa vyema kuona wanafunzi wetu wengi wakifurahia likizo ya Aprili na kushiriki katika Akademia ya Mapumziko ya Majira ya Masika. Ilikuwa bidii kuu PPSD kote kuajiri wanafunzi na wafanyakazi katika wiki pamoja na timu zinazo simamia mabasi na chakula. Wanafunzi walifurahia wiki yote na kujifunza pia.

Mwishowe, asanteni nyote ambao mlikuja kujitolea kwa Sodexo kusambaza maelfu ya vyakula kati ya shule zetu sita mnamo Jumanne. Ilikuwa inalipa kutazama vyote tulivyo weza kufanya kusaidia jumuiya yetu wakati tunapofanya kazi pamoja.

WEKA ALAMA KWA KALENDA YAKO!

○ **EID AL-FITR**
(Hakuna Shule)
Ijumaa, Aprili tarehe 21, 2023

○ **MAJARIBIO YA RICAS ELA**
Msingi: Kipindi cha 1 Darasa la 5
Kipindi cha 2 Darasa la 4
Jumatano, Aprili 19

○ **MAJARIBIO YA RICAS ELA**
Msingi: Kipindi cha 1 Madarasa 3 & 4
Middle: Kipindi cha 1 Madarasa Yote
Jumanne, Aprili 18

○ **MAJARIBIO YA RICAS ELA**
Msingi: Kipindi cha 2 Madarasa 3 & 5
Middle: Kipindi cha 2 Madarasa Yote
Alhamisi, Aprili 20

○ **MITIHANI YA SAT / PSAT**
High Schools
Jumatano, Aprili 19

APRILI MENYU YA SHULE

TAARIFA MPYA ZA WILAYA

KULA, CHEZA, JIFUNZE

Jiji la Providence, kwa ushirikiano na PPSD, inarudusha mipango maarufu ya **Kula, Cheza, Jifunze** ya msimu wa kiangazi kwa vijana katika msimu huu wa kiangazi. Mipango hii inapeana vyakula vya bure, fursa ya burudani na kazi za msimu wa kiangazi. Familia zinaweza kusajili hapa kuanzia Aprili tarehe 29 na pia wanaweza kuhudhuria Maonyesho ya Fursa za Msimu wa Kiangazi katika PCTA siku hiyo hiyo kuanzia saa nne asubuhi 10:00 a.m. hadi saa nane mchana 2:00 p.m. kujifunza zaidi kuhusu mpango Kula, Cheza, Jifunze inaweza kupeana.

USASISHO WA SURVEYWORKS

Tunafurahia kushiriki kwamba zaidi ya 39% ya familia zetu za PPSD zilikamilisha SurveyWorks mwaka huu, kupita lengo letu. Asante kwa kuchukua muda kunipatia maoni yako. Nashukuru kwa dhati. Shukrani nyingine inaenda kwa wafanyakazi wetu kwa bidii yao ya kusambaza neno kuhusu utafiti. Tunangojea kwa hamu kuchambua matoke kusaidia kuhudumia bora familia zetu za PPSD.

MAJARIBIO YA RICAS, PSAT NA SAT

Ukumbusho kwa wanafunzi na familia wa shule ya Elementary na ya Middle ya kwamba majaribio ya RICAS kwa ELA inaanza mnamo Jumanne, Aprili 18 na itaendelea hadi Alhamisi, Aprili 20. Ukumbusho kwa wanafunzi wetu wa shule za sekondari na familia ya kwamba PSAT na SAT zitafanyika mnamo Jumatano, Aprili 19. Tafadhali tembelea tovuti ya Wilaya kwa taarifa zaidi kuhusu tarehe maalum.

Join the Conversation
SurveyWorks
January 17 - March 31



Sponsored by The DEI Work Group, a partnership between the Offices of Equity & Belonging and Human Resources

Register here
(closes April 25)
All PPSD employees welcome!

april
EMPOWER MEET UP
for Educators of Color

"Definitely coming to every one of these."

DR. CARROLL MEDEIROS, M.D. FACOG
Clinical Assistant Professor, Alpert Medical School, Brown University

This month we will focus on personal wellness, public health, and how best to support our students' well-being.

Everett: Company Stage & School
9 Duncan Avenue, Providence, RI 02906
APRIL | 27th | 4:30PM

Providence Schools



Providence Schools

CULTURALLY AND HISTORICALLY RESPONSIVE EDUCATION

DR. GHOLDY MUHAMMAD
VIRTUAL COMMUNITY WORK SESSION

TEACHERS, PARENTS, ALL COMMUNITY MEMBERS WELCOME

MAY 31, 2023
3:45-5:15PM, ON ZOOM
PTU PLEASE REGISTER ON FRONTLINE FOR THIS PAID SESSION.
ALL OTHER COMMUNITY MEMBERS, PLEASE SCAN THE QR CODE TO REGISTER

OFFICE OF EQUITY AND BELONGING
EACH STUDENT EVERY DAY

COMMUNITY MEMBERS WILL RECEIVE THE ZOOM LINK UPON REGISTRATION

USAWA NA USHIRIKI

Mkutano wa emPOWER kwa Walimu wa Rangi

Usisahau kusajili katika mkutano wa mwezi huu**wa emPOWER**unao andaliwa mnamo**Aprili tarehe 27, 2023**saa kumi unusu jioni 4:30 p.m katika Everett Company Stage na Shule inayopatikana katika 9 Duncan Avenue huko Providence. Maegesho ya barabara yanapatikana katika Duncan Avenue, North Main Street, na Jenkins Street. Mgeni wetu mzungumzaji mkuu wa mwezi huu, Dkt. Carrol Medeiros, ata lenga katika ustawi wa kibinafsi, afya ya umma na jinsi bora zaidi ya kusaidia ustawi wa wanafunzi wetu. Sajili hapa! Tunatumaini kukuona hapo! Ikiwa una maswali yeyote, tafadhali wasiliana nasi katika equity@ppsd.org. Walimu wote wa PPSD wanakaribishwa kuhudhuria.

Equity Una boresha Ufadhili

Ufadhili wa Equity unawezesha wanafunzi na walimu kujaribu mawazo mapya ya ubunifu na uvumbuzi unao saidia ufundishaji na masomo bora, na pia kuboresha uelewaji na kuthamini utamaduni, kujitolea kupinga ubaguzi wa rangi na kuelewa ushirikiano wa kijamii na demokrasia. **Ufadhili wa Equity** utapeana pesa kwa miradi ya shule kati ya $500 na $4900. Jifunze zaidi katika muhtasari wa Uboreshaji wa Ufadhili wa Equity, na kuwasilisha ombi la Uboreshaji wa Ufadhili wa Equity, bofya hapa! Ikiwa una maswali yeyote, tafadhali wasiliana nasi katika equity@ppsd.org.

Dkt. Gholdy Muhammad, Mei 31, 2023

Jiunge nasi katika sehemu ya pili ya **warsha ya Dkt. Muhammad** kuhusu masomo yanayo zingatia utamaduni na historia. Kipindi chetu cha kwanza kilikuwa na zaidi ya wahudhuria 85 na tulijifunza njia za kushughulisha wanafunzi wetu wote, na kuthamini uzoefu wao katika masomo. Kipindi hiki kita fanyika kupitia Zoom. Walimu wa PPSD, tafadhali sajili katika Frontline, wazazi na wanajumuiya, tafadhali tumieni kiungo hiki kusajili ili kupokea taarifa ya Zoom. Tunatumaini munaweza kujiunga nasi! Ikiwa una maswali yeyote, tafadhali wasiliana nasi katika equity@ppsd.org.

KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo mazuri kila siku. Hapa kuna mifano michache.



NYUMBA YA MYAMA KATIKA MAONYESHO YA NYUMBANI YA RHODE ISLAND

Wanafunzi katika **Mpango wa Seremala wa PCTA**, kwa usaidizi kidogo kutoka kwa wanafunzi katika mpango wa Kuchomelea, walikuwa na fursa kujenga kitu kwa **Maonyesho ya Nyumba ya 2023** katika Convention Center. Mradi ulikuwa njia ya wanafunzi kujaza masaa ya masomo kulingana na kazi, na pia wakiweza kuonyesha kazi ya bidii, kujitolea, ujuzi na ufahamu wa useremala ulio fundishwa katika mpango CTE. Kwa uwiano na mada hiyo, "Bustani za Miujiza/Mafumbo," wanafunzi walijenga maonyesho kadhaa kutoka kwa mbao, kwa kutengeneza nyumba ya myama. Wanafunzi katika Mpango wa Kuchomelea walisaidia kwa mabano ya kutengenezwa kusaidia kushikilia na kutengeneza viunzi za milango. Mchakato huo ulichukua wiki sita na wanafunzi walikuwa na fursa ya kufanya kazi na shule zingine za sekondari za Rhode Island na hata pia kukutana na watu wapya, kuunda mtandao na kujadili fursa za kazi zinazoweza patikana ziku za baadaye pamoja na wachukuzi katika maonyesho. Wanafunzi watatu wa seremala walichaguliwa kuongea katika Maonyesho ya Nyumba mbele ya Bodi ya Wadhamini kuongea kuhusu uzoefu wao katika CTE. Wanafunzi hata wali tembelewa na shirika la mtaani kutazama ikiwa wangeweza kujenga nyumba ya kucheza kwa mtoto mwenye ugonjwa hatari. Kazi nzuri kila mtu, na mwendelee na kazi bora!

SPAZIANO UPANDISHAJI WA BORITI

Boriti ya mwisho katika mradi wa ujenzi mpya wa mjengo wa **Frank D. Spaziano Elementary School** ume pandishwa hadi juu ya mjengo. Wanafunzi walipata fursa ya kutia saini katika boriti la mwisho, pamoja na **Gavana Dan McKee, Meya Brett Smiley, Kamishna wa Elimu wa Rhode Island Angélica Infante-Green**, na **Mkurugenzi mkuu Dkt. Javier Montañez**. Wanafunzi na wafanyakazi wame furahia sana kuweza kusoma katika mjengo mpya pindi utakapo malizwa wakati wa msimu wa vuli.



WIKI YA UFAHAMU WA ELIMU

Wiki ya kwanza kamili ya Aprili iliashiria Wiki ya Ufahamu wa Elimu, na **George J. West Elementary School** ili tembelewa na baadhi ya wageni kwa Siku ya Uongozi ya Mafanikio ya Wanafunzi Vijana wa RI Leaders Day. Ilikuwa siku ambayo ilileta pamoja walimu, biashara na wanao jitolea pamoja kusaidia kusherekea Wiki ya Ufahamu wa Elimu. Wageni wana jumuisha **Gavana McKee, Meya Brett Smiley, Kamishna Angélica Infante-Green, na Kanali Chifu wa Polisi wa Providence Kanali Oscar Perez**. Shukrani maalum kwa **Mafanikio ya wanafunzi vijana wa RI**kwa kusaidia kufanya hii iwezekane. Shukrani kwa kila mtu aliyetembelea!

BANDFEST

Wikendi iliyopita**Bendi ya Mount Pleasant High School** walishindana katika tamasha inayojulikana kama BandFest. Walipata alama ya juu zaidi ya 37.5 kati ya 40. Bendi hiyo pia ilifanya maonyesho pamoja na wanafunzi Barrington High School, na bendi hizi mbili ziki jumuishwa zina tengeneza Bendi Iliyounganishwa kikamili, inayo jumuisha wanafunzi kutoka Mipango ya Kipekee ya Huduma za Watoto katika shule zote mbili. Hongera kwa kila mtu aliyehusika!

KUANGAZIWA KWA MWANAFUNZI

Pata kufahamu wanafunzi wetu wakubwa hodari Wilayani!

Nevaeh Seales
Senior, Central High School
MS: Nathanael Greene Middle School
ES: Mary E. Fogarty Elementary School

Ida Faye
Senior, Central High School
MS: Nathanael Greene Middle School
ES: Robert F. Kennedy Elementary School

Anthony Aldana
Senior, Central High School
MS: DelSesto Middle School
ES: Frank D. Spaziano Elementary School

> Jishughulishe! Hii ndiyo njia utakayo pata raha nyingi.”

Mipango yako ni gani baada ya shule ya sekondari?

NS: Mwaka ujao, napanga kwenda hadi CCRI kwa sababu haina malipo, kwanza. Pia nataka kupokea hizi alama ili niweze kujisafirisha hadi kwa shule ya miaka nne na bado nikiokoa pesa. Sina uhakika ni shule gani napendelea zaidi ya CCRI.

IKIWA: Bado nafanya maamuzi kati ya vyuo. Itakuwa aidha Bryant au Chuo cha Rhode Island (RIC).

AA: Bado nafanya maamuzi pia. Kwangu mimi, ni kati ya Bates, Middlebury, au Chuo cha Boston.

Je, ulipata uzoefu gani ukiwa Central? Kwa nini uli chagua kwenda Central? Ni nini utakacho kosa?

NS: Kwa ukweli siku anzia Central. Mwanzoni nilianza Classical, halafu nikahamia Georgia. Halafu nikarudi Rhode Island. Central ilikuwa karibu na nyumba yangu.

IKIWA: Ilikuwa kitu sawia kwangu. Nili chagua Central High School kwa sababu ilikuwa karibu na nyumbani kwangu. Nilitaka kwenda kwa moja ya hizi shule tatu: Central, PCTA, au Classical. Nilifurahia sana. Tuko na darasa dogo. Ni 250 tu au karibu na hiyo. Kwa sababu hiyo, tume karibiana.

AA: Iko karibu na nyumbani kwangu pia. Mimi pia siku fahamu kiingereza sana kwa hivyo siku fahamu fursa zingine, kwa hivyo siku wasilisha ombi kwa shule zingine.

Shughuli zako za mtaala ziada ni gani?

NS: Sisi sote watatu tuko katika Baraza la Wanafunzi, nadhani kwa sababu ya kampeni ya Ida. Ilinichochea kwamba tunaweza badilisha hii shule na kuifanya ipendeze zaidi.

IKIWA: Sote tuko katika Baraza la Wanafunzi. Kwa hivyo tunasaidia kupanga matukio. Sasa tuna panga tamasha yetu. Tuna panga wiki za moyo zetu. Anthony na mimi tuko katika Klabu cha Vitabu, na Neveah na mimi tuko katika Klabu cha Umaridadi. Nilicheza tenisi. Niliipenda. Nitakosa jumuiya, michezo ya kandanda na usiku za NUA. Nilifurahia Baraza la Wanafunzi. Tukio langu nililopenda zaidi ni kupanga rangi uso za wanafunzi wenzangu kabla ya mkutano wa hadhara wa motisha. Mikutano yetu ya hadhara ya motisha yana furahisha.

AA: Mimi ni mshiriki wa Klabu cha Sataranji, NUA na Baraza la Wanafunzi.

Ni mfanyakazi gani amekuwa na athari kubwa kwako?

IKIWA Bw. Lacouture, mwalimu wetu wa Hisabati alikuwa na athari kubwa kwetu. Alikuwa ni mtu unayeweza kumkaribia na kuongea naye. Daima alipatikana kuongea, hata baada ya darasa. Alikuwa ana chekesha na ali furahisha darasa lake.

NS: Ninakubali. Yeye ni mwalimu bora zaidi. Hususan kwa sababu nilikuwa mgeni na daima alinifanya nihisi nimekaribishwa.

Ni ushauri gani uko nao kwa wanafunzi wapya wanaojiunga?

NS, IF, AA: Jishughulishe! Hii ndiyo njia utakayo pata raha nyingi.

NS: Sio ngumu kujishughulisha. Pindi unapopata umati unao taka kuwa karibu nao.

Ni jambo gani unao ogopa zaidi baada ya kuhitimu?

IKIWA Kutopata usaidizi hapo. Katika shule ya sekondari uko na usaidizi kati yako. Katika dunia halisi, ni lazima ujitafutie.

NS: Nakubaliana na Ida. Lakini naogopa tu. Nahisi kama sina ujanja wa dunia. Nina wasiwasi nitaishia kukosa pesa au kuwa kwa madeni.

AA: Ningesema sijui ni nini kinachofuata. Nina wasiwasi kiasi kuwa wa kwanza katika familia yetu kwenda chuoni.

NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Shule 6 za Providence zinapeana chakula cha bura kwa wanafunzi
  ABC6, Aprili 11
- Kula, Cheza, jifunze: Mpango mashuhuri kwa watoto wa shule za Providence kurudia msimu huu wa kiangazi
  WPRI, Aprili 4

WILAYANI

SIKU YA CHUO KATIKA BROWN

Wanafunzi wengi wa PPSD walihudhuria **Siku ya Brown University College** hivi majuzi. Wanafunzi wako na fursa ya kusikiliza **Meya Smiley, Kamishna Angélica Infante-Green, Mkurugenzi mkuu Dkt. Javier Montañez,** na wanafunzi wa sasa wa **Brown University na** walimu kuhusu maisha ya chuoni. Wanafunzi wa PPSD wamekuwa na fursa ya kuchunguza nafasi tofauti katika chuoni na kupata mtazamo wa jinsi maisha ya chuoni yanaweza kufanana. Shukrani kwa kila mmoja aliyefanya hii iwezekane kwa wanafunzi wetu!

AKADEMIA YA MAPUMZIKO YA MAJIRA YA MASIKA

Shukrani kubwa kwa wanafunzi na wafanyakazi wetu wote ambao walishiriki katika Akademia ya Mapumziko ya Majira ya Masika wakati wa likizo ya Aprili. Tumekuwa na wanafunzi wengi walioshiriki, kuwasaidia kuwatayarisha kwa RICAS, PSAT, na SAT wiki ijayo. Wanafunzi wali shughulika kabisa na wafanyakazi walifanya masomo yafurahishe na kusaidia wanafunzi. Bahati njema kwa wanafunzi wetu wote katika majaribio yao wiki ijayo!

WIKI YA KITAIFA YA WALIMU WAKUU WASAIDIZI

Hivi majuzi tulisherekea **Wiki ya Walimu Wakuu Wasaidizi**, na hapa PPSD, tuko na bahati kuwa na Walimu Wakuu Wasaidizi hodari sana. Wanasaidia kuhakikisha kwamba siku za shule zinaendelea bila hitilafu, kuhakikisha usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wetu, wanashirikiana na familia na zaidi sana. Tunashukuru sana Walimu Wakuu Wasaidizi wetu hodari ambao tuko nao hapa Wilayani, na tuna wathamini nyote. Asanteni nyote kwa kazi mnayo fanya!

USAMBAZAJI WA CHAKULA BILA MALIPO

Sodexo, pamoja na wanafunzi na wafanyakazi kutoka PPSD, walipeana chakula cha bure katika maeneo tofauti hii wiki iliyopita kwa watoto wenye umri wa miaka 18 na chini. Usambazaji wa chakula ulifanyika katika shule zetu sita. **Asa Messer Elementary, Gilbert Stuart Middle School, DelSesto Middle School, Feinstein Elementary katika Broad Street, Nathanael Greene Middle School,** na **Roger Williams Middle School**. Kila eneo lilikuwa na watu wengi waliojitolea, na watu wengi walitokezea kwa usambazaji wa chakula. Shukrani kwa kila mtu aliyejitolea kusaidia hii iwe na mafanikio makuu!

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima, na tunataka kueneza ujumbe! ikiwa una programu, hafla, mfanyakazi, au mwanafunzi mwenye hadithi nzuri ajabu ambayo ungependa kuonyesha, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.

Providence Schools

© 2023 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org